Katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* mtunzi amenukuu na kurejelea baadhi ya mistari na maneno kutoka kwenye Biblia. Mazungumzo ya John Okello na wapambanaji wenzake yanatubainishia hili:

OKELLO: Usiku wa jana; Mwenyezi Mungu kanionesha katika maono: nyota kubwa. Kimondokikitokea Tanganyika, kikaseleleka angani na kuzama Zanzibar, ndani ya bahari ya Hindi.

OKELLO: Mmesikia? Mbingu zimetulia. Maana yake ni kuwa Field Marshall wa mbinguni, ushindi ametupatia (anaita) Mfaranyaki! Chanzo: *Sadaka ya John Okello* (Uk. 42).

Katika tamthiliya hii, John Okello amechorwa kama nabii wa Mwenyezi Mungu katika mazungumzo hayo hapo juu. Nabii ni mtu anayetumia nguvu za kiungu kunena maagizo na hukumu alizopewa na Mwenyezi Mungu atoe kwa wanadamu; mtume (BAKITA, 2022). Wanazuoni hawa wanaendelea kueleza kuwa, nabii ni mtu ambaye Mwenyezi Mungu kwa kutumia uweza wake, humfunulia mambo ya wakati uliopita au ujao na kumwamuru kuyasema au kuyaandika kwa faida za wanadamu. Kimsingi, nabii ni mtu mwenye mamlaka, ambaye Mola

amemjaalia maono akaona mambo yanayotukia katika ulimwengu mwingine. Watu waonao maono ni manabii wa Mwenyezi Mungu. Katika Biblia watu hawa wamejitokeza na mara nyingi walitumika pia nyakati za vita katika masimulizi mbalimbali ndani ya Biblia. Manabii hawa hutangulia mbele na kusema na watu mambo yatakayojiri kuhusu vita au tukio hilo lililo mbele ya jamii kwa wakati huo.

Samweli ni mfano wa watu wenye maono katika Biblia. Kijana huyu alikuwa mcha Mungu na alikuwa akitumika chini ya Mzee mmoja aitwaye Eli. Siku moja alipokuwa usingizini alipata maono kuhusu bwana wake, Mzee Eli. Alipoyaona maono hayo kesho yake alimwambia mzee wake juu ya yote aliyooneshwa na Mwenyezi Mungu kumhusu mzee huyo, alipaswa kufanya kitu kutokana na maagizo ya Mwenyezi Mungu ambayo kijana huyu aliyaona. Biblia inasema:

Naye, Samweli akalala hata asubuhi, akafungua milango ya nyumba ya Bwana. Samweli akaogopa kumjulisha Eli maono hayo.” Chanzo: Biblia Takatifu (1Samweli 3:15)

Katika kisa hiki, kijana huyu mcha Mungu anaonyeshwa maono kuhusu familia ya kiongozi wake wa kanisa. Mambo yatakayotukia na ghadhabu ambayo Mwenyezi Mungu ameipata kutokana na vijana wa Mzee Eli kutenda dhambi. Utafiti ulibaini namna nukuu hizi zilivyogeuzwa ama kubadilishwa lakini zikirejea dhana ile ile ya msingi, ya uungu na uonaji wa maono kuhusu matukio yatakayotukia hapo mbele. Mahala pengine mhusika mkuu John Okello katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* amesema maneno haya, “Kazi aliyonituma baba imekamilika.” (uk.56). Matini hii inatoa mwangwi wa maneno ya Yesu akiwa msalabani alipomaliza kazi ya kumkomboa mwanadamu kama inavyoelezwa kwenye *Biblia*. *Biblia* imeandika hivi; “Baada ya hayo, Yesu, hali akijua ya kuwa yote yamekwisha kumalizika ili andiko litimizwe, akasema, naona kiu...alipokwisha kuipokea ile siki akasema, Imekwisha. Akainama kichwa, akasalimu roho yake.” (Yohana 19: 28-30).

Nukuu hizo kwa mujibu wa makala haya zinaakisi mwangwi wa Biblia katika tamthiliya hii ya *Sadaka ya John Okello*. Kwa hivyo ni ukweli bayana kuwa upo mwangwi wa Biblia katika matini hii. Nadharia ya Mwingilianomatini inadai kuwa matini za fasihi huwa zinanukuu, kugeza au kurejelea kwa njia moja au nyingine matini nyingine tangulizi. Kwa hivyo matini uhusianona kuingiliana kwa namna mbalimbali.

3.5 Matumizi ya Ushairi

Utanzu wa kishairi umetumika pia katika kazi hizi za fasihi tulizosoma. Katika makala haya tumebainisha jinsi ushairi ulivyojitokeza na namna unavyoakisi Ubiblia katika kazi hizi za Emmanuel Mbogo. Mnyampala (1970) anasema kuwa ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale ndicho kitu kilicho bora sana katika maongozo ya dunia kwa kutumia maneno ya

mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalum. Mwanazuoni huyu anaegemea zaidi katika mkondo wa ushairi wa kimapokeo, ambao kwake msingi mkubwa ni urari wa vina na mizani. Mulokozi na Kahigi (1982:25) wanasema kwamba “ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalum na fasaha na wenye muwala, kwa lugha ya picha, sitiari au ishara katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo ili kuleta wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisia fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo.

Katika makala haya tunayoandika, tunapata mwanga kuhusu dhana hii ya ushairi inayotuongoza katika uchambuzi huu. Hivyo, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa ushairi ni kazi ya sanaa yenye kuandikwa au kuimbwa kwa kufuata kanuni za ushairi au kutofuata kanuni za ushairi. Jambo lingine la msingi linalosisitizwa katika utungo wa kishairi ni kubeba ujumbe fulani mahsus. Tumekwisha kudokeza hapo kwanza kuwa, Biblia ni kitabu kitakatifu kinachotumiwa na waumini wa dini ya Kikristo katika mafundisho ya imani yao. Wanazuoni katika uga wa fasihi wanakubaliana kuwa kitabu hiki ni miongoni mwa mazao makubwa sana ya fasihi ambayo ni vigumu kuchujuka uzuri wake. Metzger na Coogan (1993) wanaelezea *Biblia* kama kitabu chenye kufasiliwa kama fasihi. Ubora wa fasihi ya *Biblia* umechangiwa na maudhui yake, lugha ya kishairi na ujuzi wa maandishi wake katika kufasiri kazi hiyo. Aina kuu za fasihi zinazojitokeza kwenye *Bibliani* nathari na ushairi. Baadhi ya vitabu katika Biblia vilivyotumia mtindo wa ushairi ni Zaburi, Mithali, Wimbo Ulio Bora na Ayubu.

Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*, imetumia mtindo wa kishairi, ambao umegeuzwa kuendana na muktadha lakini pia ukahusianishwa na mawaidha au maneno ya Mwenyezi Mungu. Kwa sehemu kubwa katika Onyesho la Tisa la *Nyerere na Safari ya Kanaani*, mtunzi amempa lugha ya kishairi mhusika mkuu Nyerere alipokuwa akiongea na hadhara Ikulu. Tunaposoma beti hizo Ubiblia unajitokeza. Baadhi ya beti zenye mwangwi waBiblia katika masikio ya wasikilizaji na macho ya watazamaji ni hizi:

3. Humu ndani ya mwili, kuna moyo umetulia,
Wengine wamwita Roho, udongoni umejikalia,
Roho anao uhai, uzima mwili kuugawia,
Itajengwa na wenye moyo, hii yetu Tanzania.

4. Nakuuliza ewe mwili, ni lipi unaloringia,
Ama ni wako ukwasi, na wingi wa zako rupia,
Hata Roho akikushauri, ubishi meng'ang'ania,
Itajengwa na wenye moyo, hii yetu Tanzania.

5. Utaingia hasara, Roho kumpuuzia,
Anazo hekima lufufu, aweza kukutunukia,

Roho yako ni 'mungu', kiungo cha wako Jalia,
Itajengwa na wenye moyo, hii yetu Tanzania.

Chanzo: *Nyerere na Safari ya Kanaani* (Uk.61-64).

Katika shairi hili mtunzi anamhusisha mhusika Roho na kubainisha utendaji wake kama anavyoeleza kwenye Biblia. Roho inarejea kile ambacho huupa mwili wa mwanadamu uhai ndiyo kusema bila roho, mwili umekufa (Yakobo, 2:26). Mbogo anawakumbusha viongozi kufanya kazi kwa unyenyekevu. Wasijivunie nafasi zao na kutesa watu wa chini kwani wao pia ni wanadamu, muda wowote Mola anaweza kuondoa huyo Roho anayewapa watu uhai, wakafariki. Pia, tunaposoma tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* tunakutana na mtindo wa kishairi kutumika. Mtunzi Emmanuel Mbogo ametumia maghani katika kazi yake hii. Mtindo huu wa kishairi umetumika kwa sehemu sehemu ndani ya kazi:

IDDI: Field Marshall John Okello!
Mimi shujaa Iddi.
Ninaranda, ninatamba, ninatanda
Ninatambaa! Ninasambaa.
Mimi Shujaa Iddi, mwana wa Chipoko
Mimi Iddi, mwana wa mamaangu Mwajuma
Mimi niliyekataa kuja duniani
Wakati wangu ulipotimu!

Chanzo: *Sadaka ya John Okello* (Uk. 22)

Katika onesho hili, waghani wawili wanajibizana. John Okello na Idd. Mtindo huu ni maarufu sana katika kitabu cha Biblia. Vipo vitabu kabisa (tumevitaja huko juu) ambavyo vimeandikwa kwa mtindo wa kishairi mwanzo hadi mwisho. Baadhi ya hivyo ni *Zaburi* na *Wimbo Uliobora* zilizoimbwa na Mfalme Daudi na Mfalme Suleiman. Hii pia inadhihirisha Ubiblia katika kazi za Emmanuel Mbogo.

4.0 Hitimisho

Makala haya yamebainisha kwamba kuna Ubiblia uliojibainisha katika tamthiliya teule za *Sadaka ya John Okello* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*. Ubiblia huo umejitokeza kwa namna mbalimbali. Mwandishi kuchukua baadhi ya masimuliziyaliyomo ndani ya Biblia kujenga kisa cha kazi yake, wahusika, kutumia nukuu za Kibiblia, mitindo ya Kibibliana dhana mbalimbali zilizomo katika Biblia. Mwangwi waBiblia katika kazi hizi unasikika kwa mtu yeyote aliyepata kukutana na Biblia. Matukio, ujenzi wa visa na mtindo wa mazungumzo ya wahusika unaendana sawasawa na yale yaliyojiri kwenye Biblia kama tulivyobainisha wakati tukijadili na kubainisha mwangwi wa Biblia katika kazi hizo teule. Washadidi wa nadharia ya Mwingilianomatini, wanadai kwamba matini za fasihi hurejelea kwa njia moja au nyingine matini nyingine tangulizi. Mhimili huu unaegemezwa kwenye kuamini kuwa kazi ya fasihi ni matini mpya ambayo

haijitegemei yenyewe. Matini mpya lazima ihusiane na matini nyingine zilizotangulia. Ubiblia unaojithiirisha katika tamthiliya teule za Mbogo.

Marejeleo

BAKITA (2022). Kamusi Kuu ya Kiswahili (Toleo la 3). Dar es Salaam: Longhorn Publishers Plc. Tanzania.

Chakaipa, P. (1967). *Dzasukwa Mwana-Asona-Hembe*. Salisbury: Longman.

Chidzero, B. (1957). *Nzvingamustsvairo*. Salisbury: Longman.

Edson, T. Z. (2016). Historia ya Tamthiliya ya Kiswahili Nchini Tanzania Tangu Kuanza Kwake Hadi Hivi Sasa (Mhadhara Darasani). Mwanza: Chuo Kikuu cha Mt. Agustino.

Herman, L. B. (2011). “Dhima ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili.” Makala katika *Kioo cha Lugha* (Juz.9). Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kipacha, A. (2017). *Uchuro katika Nathari Teule za Euphrase Kezilahabi*. Swahili Forum (Vol. 24): 1 – 15.

Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*. New York: Columbia University Press.

Lema, E. P. (2010). *Religion and Fanonist Marxism: The Study of Ngugi's Four Novels* (MA. Literature Thesis). Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Hisaniel, M. (2012). *Sadaka ya Mavuno: Mara Tatu kwa Mwaka*. KKKT-DMP, Dar es Salaam.

Jamaadar, A. (1978). *Mui Huwa Mwema*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Kiprotich, P. J. (2013). *Mchango wa Mbazi za Biblia katika Ukuzaji wa Fasihi Andishi ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenya.

Madumulla, J. (1993). Mwandishi wa Kiswahili na Suala la Ukweli wa Maisha: Fasihi Andishi na Uchapishaji. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mapara, J. (2003). *The Bible and Literature: A case study in Shona novels* (Ma Thesis). Harare: University of Zimbabwe.

Massamba, D. P. B. (2003). “Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili.” Katika *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili (III), FASIHI*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbogo, E. (2015). *Nyerere na Safari ya Kanaani*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

- Mbogo, E. (2015). *Sadaka ya John Okello*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
- Metzger & Coogan (1993). *The Oxford Companion to the Bible*. New York: Oxford University Press.
- Mlaga, W. K. (2010). *Historia ya Tanzania Kuanzia 1960-1980 katika Riwaya Teule za Kiswahili: Uhakiki wa Kihalisia* (Tasnifu ya Uzamili). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Mningo, R. A. (2015). *Tathimini ya Mwingilianomatini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liyongo* (Tasnifu ya Uzamili). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mulokozi, M. & Kahigi, K. (1982). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Musengezi, G. H. (1984). *Zvairwandza Vacara*. Harare: Zimbabwe Publishing House.
- Msangi, E.O. (2018). *Kuchunguza Ubiblia katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo* (Tasnifu ya Uzamili). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Plottel, J. P. and Charney, H. (1978). Intertextuality: New Perspective in Criticism. *New York Literary Forum, Vol. 2*: +306 pp.
- Somba, J. (1969). *Alipanda Upepo na Kuvuna Tufani*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
- Soseleje, M. (1946). *Safari ya Msafiri*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Tsodzo, T. K. (1993). *Mudhuri Murefu Murefu*. Harare: Longman Zimbabwe.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Nafasi ya Fasihi - Mazingira Kuelekea Uchumi wa Viwanda Nchini Tanzania: Mifano Kutoka Katika Nyimbo za Mrisho Mpoto na Beka Flavour

**By
Rose Sekile**

Chuo Kikuu Katoliki Mbeya
rosesekile80@gmail.com

Ikisiri

Makala haya yamechunguza nafasi ya fasihi mazingira katika kuelekea uchumi wa viwanda nchini Tanzania. Data za msingi zilipatikana katika jamii kwa kuchunguza nyimbo zinazohusu mazingira. Mbinu ya usomaji makini na upembuzi yakinifu zilitumika kupata data za msingi. Mihimili ya nadharia ya Uhalisia na nadharia ya Ekolojia ndiyo iliyoongoza katika mjadala wa uchanganuzi wa data zilizowasilishwa. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya mazingira na uendelezaji wa viwanda. Aidha, nyimbo ni nyenzo muafaka ya kuelimisha jamii kuhusu utunzaji wa mazingira na kudhibiti mienendo na tabia isiyofaa katika jamii. Utunzaji wa mazingira nchini Tanzania inaonekana ni jukumu la asasi zilizopewa dhamana kuhusu mazingira na si jukumu la kila mmoja wetu. Makala haya yanapendekeza kuwa ni vyema uelimishaji wa elimu mazingira ufanyike katika ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya kaya hadi kitaifa ili kumfanya kila mmoja wetu awe sehemu ya utunzaji wa mazingira. Uanzishwaji wa viwanda na ukuaji wa uchumi unatakiwa uende sanjari na uhaishaji wa mazingira.

Istilahi muhimu: Mazingira, Fasihi - mazingira, ekolojia, uchumi na uchumi wa viwanda

1.0 Utangulizi

Makala haya yanachunguza nafasi ya fasihi - mazingira kuelekea uchumi wa viwanda nchini Tanzania. Thirmurthy (2004) anasema kuwa mazingira ni vitu vyote vilivyo hai na visivyo hai vinavyomzunguka binadamu. Aidha, anaendelea kufafanua kuwa mazingira ni pamoja na maliasili zinazopatikana katika maeneo tunayoishi, hewa, ardhi na maji, uhai wa mimea na wanyama, hali ya kijamii, pamoja na kiuchumi. Mambo mengine ni hali inayoshawishi maisha ya binadamu na jumuiya zao, majengo, miundo-mbinu, mitambo na mambo mengine yaliyoundwa na wanadamu, mada ngumu, vimiminika, joto, sauti, mitetemo, mnururisho wa moja kwa moja na ule unaotokana na shughuli za kibinadamu au mchanganyiko wa mahusiano ya vyote vilivyotajwa hapo juu. Fasihi- mazingira ni uwanja unaojadili dhana ya kimazingira katika fasihi na sanaa nyingine. Uwanja huu unachukua mkabala wa wahusika wanavyohusiana na ekolojia, maudhui ya ekolojia na jinsi lugha inavyovyazwa na ekolojia.

Pia, ni maandiko ya kitaalamu yanayoeleza kuhusu maudhui yahasu mazingira, hususani yanayofafanua mahusiano yaliyopo kati ya binadamu, jamii na mazingira. Payne na Barbara (2010) wanasema kuwa uwanja huu unachukua mwelekeo wa kimwingiliano taaluma kwa

kuhusisha usomi wa mandhari, nyanda na sehemu za dunia kuoanisha na sanaa mbalimbali. Fasihi- mazingira katika Fasihi huchunguza na kutalii uhusiano uliopo kati ya matini ya kifasihi na mazingira asilia, maarubu ya mazingira asilia katika vitushi vya sanaa. Thamani ya kimazingira anayowasilisha msanii endapo inawiana na maarifa ya kiikolojia na inachunguza tofauti za kimazingira za sanaa za mwanaume na mwanamke. Pia, inachunguza athari za fasihi - mazingira kwa hadhira yake na namna mazingira yanavyojipenyeza katika fasihi. Mwisho, inachunguza mwingiliano unaojitokeza baina ya masimulizi ya mazingira, mapisi, falsafa, maadili, saikolojia, anthropolojia, utamaduni na fasihi (Nabeta, 2014). Kazi zenye mlengo huu, hujadili pia namna ujumi wa kifasihi uliomo kwenye kazi za fasihi unavyodhihirisha jinsi tamaduni za jamii zinavyoimba kudhibiti na kuukilia mitazamo, imani, elimu, na ufahamu kuhusu mazingira.

Ekolojia ni taaluma inayochunguza kuhusu mifumo na dhana ya maumbile kiasilia. Dhima ya mifumo ya ekolojia huathiriana na jinsi binadamu anavyohusiana na mazingira yake (Odun, 1971). Pia, ni sayansi inayochunguza uhusiano uliopo kati ya viumbe hai na mazingira wanayoishi. Ekolojia inajaribu kutabiri mabadiliko yanayohusiana na shughuli za wanadamu. Duniani kote, tafsiri pana ya viwanda inajumuisha uchimbaji wa madini na mawe, utengenezaji wa bidhaa na huduma za uzalishaji na usambazaji wa maji, usimamizi wa maji taka, taka nyingine na shughuli za kurekebisha uharibifu wa mazingira na ujenzi. Ujenzi wa uchumi wa viwanda ni kufanya mageuzi ya kimfumo, kijamii na kiuchumi yanayotawaliwa na teknolojia na kuongeza uzalishaji yanayofanya viwanda kuchangia zaidi katika ukuaji uchumi. Maendeleo ya viwanda yanachangia sana uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Uanzishaji wa viwanda ni jambo zuri ili kufikia uchumi wa thabiti, ingawa hatua makini zisipotekelzwa kwa uangalifu linaweza kuharibu mazingira na uhai wa viumbe hai. Makala haya yamechunguza nafasi ya fasihi mazingira katika kuelekea uchumi wa viwanda nchini Tanzania.

2.0 Nadharia na Mbinu za Utafiti

Makala haya yamechunguza nafasi ya fasihi mazingira katika kuelekea uchumi wa viwanda nchini Tanzania. Data za msingi zilipatikana katika jamii kwa kuchunguza nyimbo zinazohusu mazingira. Mbinu ya usomaji makini na upembuzi yakinifu zilitumika kupata data za msingi. Mihimili ya nadharia ya Uhalisia na nadharia ya Ekolojia ndiyo iliyoongoza katika mjadala wa uchanganuzi wa data zilizowasilishwa. Nadharia ya Ekolojia iliasisiwa na Glotfelty (1995) nchini Marekani. Ajenda kuu ya nadharia hii nikuyachunguza na kushughulikia masuala yanayohusiana na mazingira. Mara nyingi matatizo ya kimazingira yanayowasilishwa katika kazi za fasihi yanachukuliwa kuwa ni athari zinatokana na shughuli za kibinadamu. Hali hii inatokea pale shughuli za kibinadamu zinapoharibu uwezo wa kawaida wa dunia kuwezesha uendeleu wa mifumo ya ekolojia. Pia, inahusika na dhima ya mazingira katika kuukilia utamaduni wa jamii katika kipindi mahususi cha kihistoria, pamoja na mila na desturi zinazohusishwa au

zisizohusishwa na hali ya mazingira. Katika makala haya nadharia hii imetumika kuichunguza nafasi ya fasihi katika kuendeleza uchumi wa viwanda nchini Tanzania.

Pia, nadharia ya Uhalisia iliyoasisiwa karne ya 19 na kufafanuliwa zaidi na Goffman (1952), Hegel (1971) na Lukacs (1979). Uhalisia unasisitiza zaidi usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Wanauhalisia wanaona kwamba kazi ya fasihi inapaswa kuwa sahihi, iliyo wazi na inayozingatia masuala halisi bila ya kupiga chuku. Wanauhalisia wanasema kuwa msanii anapaswa kuteua, lakini akiwa na nia ya kuendeleza masuala yake kama yanavyowahusu watu katika hali halisi za maisha. Katika makala haya, nadharia hii imetumia kuchunguza uhalisia wa mazingira ya sasa na jinsi yanavyosawiriwa na mtunzi sambamba na maudhui yake. Pia, imechunguza na kudhihirisha ukweli wa kile alichokisawiri mtunzi anapochunguza uhusiano wa asih na mazingira.

3.0 Uwasilishaji na Uchambuzi

Makala haya yamechunguza nafasi ya fasihi mazingira katika kuelekea uchumi wa viwanda nchini Tanzania kwa kurejelea nyimbo za Mrisho Mpoti na Beka Flavour. Makala haya yamechunguza uhusiano wa nyimbo na mazingira asilia, taswira halisi ya mazingira katika nyimbo na mchango wa nyimbo katika utunzaji wa mazingira na kuinua uchumi wa viwanda kama ilivyoielezwa katika sehemu inayofuata.

3.1 Uhusiano wa Nyimbo na Mazingira Asilia

Fasihi kama taaluma ina uhusiano wa kiutegemezi au kiutegemeano na mazingira. Fasihi hususani nyimbo hutumia vitu mbalimbali vilivyo katika mazingira kufikia dhima yake. Msanii anaposana kazi yake hupata maarifa kutoka katika mazingira. Nyimbo ni nyenzo muafaka inayotekeleza mambo yanayotokana na msukumo wa hali halisi ya maisha. Hegel (1971) anasema kuwa kazi ya fasihi inatakiwa kutekeleza mambo kutokana na msukumo wa hali ya maisha wanamoishi. Mtunzi anatakiwa atoe usimulizi ambao unajikita katika kusimulia ukweli unaofahamika katika maisha ya binadamu. Hakuna sanaa inayojipambanua nje ya maisha ya mwanadamu, hata kama ikitokea maudhui yake yakawa katika historia ya mambo yaliyopita, sharti yatafumuwa katika fani inayopambanua maisha halisi (Okpewho, 1992). Fasihi ni uhalisia unaotokana na shughuli za binadamu ambazo hufanywa kila siku na matukio ya kweli na yenye uhalisi. Binadamu ndio wanaoshiriki katika shughuli za kila siku katika maisha na maendeleo ya jamii. Beka Flavour katika wimbo wa 'Mazingira' anaeleza:

Kuyatunza mazingira ni wajibu wa kila Mtanzania,
Tena bila kufosiwa, majumbani tunamoishi wenyewe,
Tuelimishane kuhifadhi mazingira, vyanzo vya maji tuvilinde,
Tuviheshimu na tuvitunze, tuvipende hivyo ni vitu muhimu,
Na baharini tusiende kutupa takataka, samaki waringe nyumba,

Yao ya maisha, wavuvi pia mjifunze kuacha uvuvi haramu, mabomu,
Ya nini kwenye maji kama mna vita na Vietnam na viwandani chonde,
Chonde moshi huharibu mazingira na maji taka vile vile si mazuri,
Kwetu binadamu, tutapiga hatua tukiungana kuyatunza mazingira.

Binadamu ana uhusiano na mwingiliano mkubwa na mazingira yake. Uhusiano huo unaweza kuwa wa binadamu na binadamu mwenzake, wanyama na mimea. Uhusiano huu unaweza kuwa wa kijiografia kama vile misitu, mito na mabadiliko ya hali ya anga. Pia, unaweza kuwa mazingira ya kijamii kama vile shule, familia, ujirani na utamaduni. Uhusiano huu unachangia sana katika ukuaji na uendelezaji wa uchumi. Katika uhusiano, upatano na mwingiliano huu binadamu ndiye ana athari kiuchumi, kisiasa na kijamii, tofauti na viumbe vingine vyote. Odun (1971) anasema kuwa dhima ya mifumo ya ekolojia huathiriwa na jinsi binadamu anavyohusiana na mazingira yake. Tamaduni za jamii zina athari chanya au hasi kuhusu uhai wa mazingira na uchumi kwa jumla. Glotfelty (1996) anasema kuwa vitendo vinavyohatarisha maisha ya binadamu vinaweza kujengewa misingi yake kutegemeana na utamaduni wa matumizi ya mazingira asilia.

Ulimwengu umezungukwa na mambo mengi yanayosababisha uchafuzi wa mazingira. Binadamu anapoendelea kuhitilafiana na mazingira yake huathiri maendeleo yake kiuchumi, kijamii na kisiasa ambayo huibuka kila siku. Kutokana na uharibifu wa mazingira katika karne hii ya ishirini na moja, binadamu anatakiwa kuibuka na mbinu mpya za kutunza mazingira ya kiasili na jinsi ambavyo anastahili kuingiliana nayo (Claser, 2002). Ili binadamu ajielewe na kufikia uwiano kati yake na mazingira anamoishi, lazima ajielewe na kujitambua. Fasihi humfanya mtu aelewe mazingira anamoishi. Fasihi yoyote ile haikosi kufundisha jambo kimakusudi ama kisadfa. Fasihi inachora taswira ya uhalisi wa maisha ya binadamu na mazingira; na kuwasilisha hali, maingiliano, mivutano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Ntarangwi (2004) anasema kuwa kazi ya fasihi inafaa kuwaweka wanajamii katika ulimwengu wao wa kawaida wa kweli na halisi.

3.2 Taswira Halisi ya Mazingira katika Nyimbo

Taswira ni picha ya mambo au vitu inayomjia mtu akilini mwake (TUKI, 2004). Msanii ana zana zake anazitumia kuchora taswira akilini mwa mtu. Zana hizo ni uhodari wa maneno yanayopangiliwa kwa utaratibu ambao huleta mguso na mnaso kwa msikilizaji. Lugha iliyojaa usanifu, urazini na umahiri ambao ndicho chombo maridhawa cha fasihi kinachotumika kutoa ujumbe wa fanani kwa hadhira. Mazingira katika fasihi ni kitu chenye maana na umuhimu katika utunzi wa kazi ya sanaa. Msanii anapobuni kazi yake hutumia vitu vilivyomo kwenye mazingira. Vitu hivyo ndivyo hutumika kujenga taswira katika akili ya mtu (Escarpit, 1974). Ubunifu huo hufanyika wakati msanii anataka kutoa lile alitakalo ambao ulikuwa unamkereketa moyoni mwake. Senkoro (2011) anasema kuwa inategemea wahusika hao

wanawakilisha nini na wanatumiwaje katika kazi za fasihi. Sanaa yoyote inachipuka kutokana na mila na desturi zilizo katika mazingira aliyomo mtu. Fasihi simulizi lazima ichukuliwe kama ilivyo na uhusiano usiotatanika na maisha ya jamii.

Wasanii wengi, wakiwemo watunzi wa nyimbo kwenye kazi zao wanaeleza kile wanachokishuhudia kwa sasa kuhusu uharibifu wa mazingira. Sanaa zao zimeweka juhudi za wahusika kuvaa uhusika wa harakati za kutetea uharibifu wa mazingira (Njogu na Chimera, 1999). Msanii hupata msukumo wa kutunga kazi yake kutokana na matukio na mabadiliko yanayoikumba jamii katika mazingira wanamoishi. Hegel (1971) anauona ulimwengu mzima kama unaoelewa kwa kueleza na kusimulia mawazo ya kweli ambayo yanapatikana katika ulimwengu wa kihalisia. Nyimbo hazina budi kuchangia na kutoa msukumo zaidi kuchangia masuala ya kimazingira, kwa kuwa hufungamanishwa na maisha ya binadamu. Kwa mfano, wimbo wa msanii Mrisho Mpoto ulioimbwa kwenye kampeni ya mazingira ‘*Nitunze Nikutunze*’ ulitoa taswira halisi ya mazingira yetu ya sasa. Kampeni hii ilifanyika Mbagala, jijini Dar es Salaam. Kampeni hii ilikusanya watu wengi, wengi wao wakitaka kumuona msanii huyo. Ujumbe ambao aliutoa kwenye wimbo huu uliwavutia watu, wakavutika na kushiriki kuimba wimbo huo. Wimbo uliwahamasisha wananchi wainuke, wacheze nawafurahi, lakini msititizo ulikuwa ni utunzaji wa mazingira. Taswira na maneno yaliyomo ni yale yaliyo katika mazingira. Taswira iliyojengwa akilini mwao ni ya vitu walivyonyavyo, wanavyoviona na kuvishuhudia katika maisha yao halisi. Katika ubeti wa pili anasema:

Hebu angalia mashoka yanavyoangusha miti na kuacha ardhi uchi bila marejesho,
Wale wanyama wanaozurura kutafuta malisho ndiyomaendeleo?
Ile mioshi inayokesha kila kukicha katika anga ndiyomaendeleo?

Jambo la kawaida kuona viumbe hai wamehama katika mazingira yao asilia kutokana na uharibifu wa makazi yao ya awali, chanzo kikubwa kikiwa ni binadamu. Baadhi ya jamii hupenda kuchoma moto, kulima, kuanzisha shughuli za uzalishaji mali kama vile viwanda vikubwa na vidogo. Utafiti huu umebaini kuwa binadamu anapotumia teknolojia ya kisasa wakati anazalisha bidhaa viwandani, anahitilafiana na mfumo wa ekolojia. Kwa mfano, moshi unaotoka viwandani unaharibu hewa inayotumiwa na wanyama, binadamu na hata mimea. Serikali inatakiwa kuwa na mikakati madhubuti wakati wa kuanzisha viwanda ili kuhakikisha havitoi kemikali zenye sumu ambazo zinaweza kuhitilafiana na mfumo wa ekolojia. Msanii anahoji ile mioshi inayokesha kila kukicha katika anga ndiyo maendeleo? Tabia ya kutojali thamani ya mazingira inapaliliwa na tamaduni zisizojali uendelezaji wa mazingira. Utamaduni wa jamii unaweza kuchochea uendelevu wa mazingira au uharibifu wa mazingira. Msanii anasema hebu angalia mashoka yanavyoangusha miti na kuacha ardhi uchi bila marejesho. Wananchi wanatakiwa waelimishwe na washauriwe kuhusu mazingira ili taifa liweze kufikia lengo la uchumi wa viwanda.

3.3 Nyimbo katika Kuendeleza Mazingira na Kukuza Uchumi wa Viwanda

Kipury (2000) anasema kuwa nyimbo, lazima zitumike kuichambua na kuelezea falsafa ya maisha ya jamii ya watu, utamaduni, historia na maendeleo ya jamii hiyo. Watunzi wengi wa kazi za fasihi huyatumia mazingira ya kijiografia kuonesha jinsi binadamu anavyoweza kuingiliana na mfumo wa ekolojia. Mtazamo wa wana-ekolojia unamakinikia sana uhusiano baina ya binadamu na mazingira asilia. Mara nyingi, matatizo ya kimazingira yanayowasilishwa katika kazi za fasihi yanachukuliwa kuwa ni athari zitokanazo na shughuli za kibinadamu. Wamitila (2008) anasema kuwa mandhari ya kijiografia ni nguzo muhimu sana katika uchunguzi wa kazi ya fasihi hasa zile zilizoandikwa katika mkondo wa kihalisia. Nyimbo ni njia muafaka inayoweza kudhibiti mienendo, tabia, na matendo yasiyofaa katika jamii kwa sababu hukaririwa kwa urahisi. Njiru (1981) anasema kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya fasihi na amali za jamii. Fasihi mazingira inazidi kuchukua dhima mpya katika jamii kadri inavyozidi kukua kiteknolojia, ingawa dhima ya kazi za kifasihi katika jitihada za kutunza mazingira haijapewa uzito kitaaluma. Pengine, yanachukuliwa kama masimulizi yasiyo na uwezo na mashiko katika kushughulikia utunzaji wa mazingira (Ogechi, 2015). Ujumbe uliomo katika kazi za fasihi kuhusu usawiri wa mazingira, ufundishwaji na uhakiki wa kazi za fasihi simulizi kuhusu utunzaji wa mazingira ni wa muhimu sana katika kuitanabisha jamii kuhusu mazingira.

Masuala ya kiuchumi, kwa kiasi kikubwa, hushikiliwa na viongozi waliopewa dhamana na wananchi. Viongozi hawa ndio huweka sainsi kwenye mikataba ya wawekezaji bila kuzingatia suala la uhifadhi wa mazingira; huongoza mifumo ya kiuchumi na nyenzo za kuzalisha mali katika jamii. Katika ubeti wa nne anasema ‘Wizara yako ndiyo wizara mama ambayo tunaitegemea, ndiyo inashika mhimili wa nchi yetu. Tumia sauti yako mheshimiwa Waziri, tumia kalamu yako, tumia nafasi yako’. Katika utekelezaji wa mikataba ya uanzishwaji wa viwanda, viongozi wenye dhamana hawazingatii sana mfumo wa ekolojia ambao ni mfumo wenye tija katika uendeshaji wa viwanda na ukuzaji wa uchumi. Wimbo huu unaeleza namna ongezeko la watu linavyohusiana sana na uharibifu wa mazingira. Wanaikolojia wanasema kuwa, mara nyingi, matatizo ya kimazingira yanayowasilishwa katika kazi za fasihi yanachukuliwa kuwa ni athari zitokanazo na shughuli za kibinadamu. Bronfenbrenner (2005) anasema kuwa maendeleo ya binadamu ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiutamadunina kiteknolojia huathiriwa na jinsi ambavyo anaingiliana na mazingira anamoishi. Mifumo ya kiuchumi, hususani uanzishwaji wa viwanda, umekuwa na changamoto kubwa sana katika uhuishaji wa mazingira. Mfumo huu wa kiuchumi unahujumu sana mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu hauzingatii suala la mazingira.

Mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania (MKUKUTA) unatambua kuwa mazingira bora ni muhimu kwa kuleta maendeleo endelevu. Sheria ya mazingira ya mwaka 2004 imeeleza wazi wajibu na majukumu ya wadau mbalimbali, kuanzia serikali za mitaa hadi taifa,

kuhusu usimamizi wa matumizi endelevu ya mazingira, kudhibiti uchafuzi wa mazingira , utunzaji wa taarifa na takwimu za mazingira, utafiti na ushiriki wa jamii katika kutekeleza mikataba. Jamii yoyote hujijengea moyo wa kuthamini misingi ya utu, usawa, upendo, na usalama wa mazingira yake. Hivi sasa uelewa wa jamii kuhusu masuala ya mazingira umepewa kipaumbele katika kuandaa mipango ya maendeleo, ingawa jamii haina taarifa za kutosha kuhusu elimu – mazingira, hivyo basi nyimbo zitumiwe kufikisha taarifa hizo kwasababu ndizo huweza kuwafikia watu kwa urahisi na wepesi.

3.4 Mchango wa Nyimbo katika Utunzaji wa Mazingira na kuinua Uchumi wa Viwanda

Nyimbo ni mkufunzi ni mwalimu wa Fasihi mazingira. Mazingira yanahusishwa moja kwa moja na uhai wa binadamu na uhai wa taifa kwa jumla. Uchumi wa taifa unategemea sana uhai wa mazingira; hata vipengele vingi vya maisha ya mwanadamu vinategemea uhai wa mazingira. Katika jamii ya sasa, wanajamii wanasaka utajiri, huku wakiharibu mazingira yanayowatunza. Maarifa ya elimu - mazingira yanatakiwa yaelezwe kwa jamii kwa namna ambayo ni ya kawaida kwa kutumia elimu-jamii, hususan nyimbo. Katika kuelimisha jamii, mara nyingi nyimbo zinazoimbwani zile zenye mafumbo, sitiari na ishara ambazo ziko katika mazingira yao. Msanii anatumia jazanda zilizosheheni sitiari na udokezi wa kijadi unaoonesha maarifa na uelewa mkubwa wa utamaduni unaohusika. Kwa mfano, kwa kutumia nyimbo zenye mizaha na kebehi, watu hujifunza, hufurahishwa, na kuchekeshwa, hasa katika mikusanyiko isiyo rasmi kwenye jamii. Mara nyingi, njia ya kejeli au kebehi huwafikia watu kwa urahisi zaidi. Jamii ina namna yao ya kuwasiliana, yaani kutumia lugha yao ya kawaida waliyozoea kuwasiliana na ambayo nyingi, si lugha rasmi.

Uchafuzi na uharibifu wa mazingira ni matokeo halisi ya jamii lengwa. Jamii isiyotunza mazingira inahatarisha kizazi kijacho, na athari hizi huenda zikaonekana miaka mingi baadaye. Katika muktadha huu, tumebaini kuwa nyimbo zinazoimbwa na makundi maalum katika jamii zina mchango mkubwa sana katika kuhamasisha utunzaji wa mazingira ili kuweza kufikia uchumi wa kati. Nyimbo hizo zimekuwa chachu katika uendelezaji wa mazingira. Heise (2008) anasema kuwa fasihi, hususani nyimbo zina uwezo wa kujenga utamaduni utakiwao kuhusu utunzaji wa mazingira wenye manufaa kwa binadamu na viumbe wengine. Hivyo, ni makosa kuamini kuwa sayansi pekee ndiyo inayoweza kutatua suala la utunzaji wa mazingira. Fasihi ina wajibu wa kuchora jamii kama ilivyo na ni muhimu kuyaeleza mambo yaliyopo ili kuwafungua macho na kuwapevusha wanajamii. Mbinu ya kutumia nyimbo kuisitiza maudhui ni ya asili, kwani imekuwa ikitumika kwa muda mrefu katika masimulizi ya kijadi. Njia hii imetumika pia kwa miaka mingi kukaririsha watoto maarifa mapya na kuhakikisha kuwa maarifa hayo hayasahauliki kwa urahisi. Uzalendo wa mazingira unatakiwa upandwe ndani ya watoto kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vikuu, ili wanapokuwa watu wazima wawe na maarifa yanayohusisha uzalishaji mali na utunzaji wa mazingira . Elimu si rahisi sana ikianza katika hali ya utu uzima.

4.0 Hitimisho

Fasihi mazingira ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na uendelezaji wa viwanda. Matatizo yatokanayo na tabia ya nchi yanayochochewa na uchafuzi wa mazingira na uharibifu wa mazingira yangeweza kudhibitiwa kwa kutumia mafunzo ya elimu inayopatikana katika Fasihi simulizi, hususani nyimbo, kwa sababu Fasihi simulizi inaishi na watu, na inamgusa kila mmoja. Harakati za kijamii za uchafuzi na uharibifu wa mazingira hazijatolewa elimu ya kutosha itakayoweza kuwafanya wanajamii wenyewe wawe sehemu ya udhibiti mazingira. Mazingira yanapohitilafiwa, shughuli za uzalishaji nazo zinakwama. Shughuli za kiuchumi zinapaswa kusaidia hifadhi ya mazingira, ikiwa ni pamoja kuhakikisha kuwa mifumo ya ki-ekolojia na mahitaji ya msingi ya ustawi wa jamii vinalindwa. Pia, ukombozi wa fikra-mazingira ufanywe kupitia elimu jamii kuanzia ngazi ya kaya. Kila mmoja ajione kama sehemu ya mazingira. Ukombozi huu huanza kwa lugha ya mazungumzo, si kwa maandishi. Mulokozi (2017) anasema kuwa, inasemekana sisi Waafrika hupenda sana kuongea, labda ndiyo maana hatupendi kusoma na kuandika. Kuongea huku kwa namna ya kawaida kwa kutumia mawasiliano ya ana kwa ana hutuvutia zaidi. Wadau wote wapewe fursa ya kutoa michango na kupata mrejesho wa masuala ya mazingira, kwani yanaweza kuchochea na kusaidia changamoto katika usimamizi na utunzaji wa mazingira yao. Katika utafiti huu tumebaini kuwa kiperi cha nyimbo kinasaidia kuelimisha jamii na wawekezaji kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Kwa hakika, kama zinavyodai nadharia za uhalisia na ekolojia, jamii inatakiwa ielezwe kwa uhalisi wake ili kuleta mabadiliko ya kimazingira. Watu wakila tabaka wanatakiwa kuchochewa ili kubadili fikra zao kuhusu suala zima la mazingira na ukuaji wa uchumi.

Marejeleo

- Bronfenbrenner, U. (2005). *Making Human Being Human Biological Perspectives on Human Development*. London: Sage Publications Limited.
- Claser, M. (2002). *Human and Nature Interaction in the Anthropocene Potential of Social – Ecological system Analysis*, Makala kutoka <http://www.oekm.de>.
- Glotfelty, C., & Fromm, H. (1996). *The Ecocritical Reader*. London: New York Routledge.
- Hegel, G.W. (1971). *Introduction to Aesthetics*. Clarendon: Oxford University Press.
- Heise, U.K. (2008). *Ecocriticism and Transnational Turn in American Studies*. Imechukuliwa May, 2022 katika www.muse.jhu.edu/journals/alh/summary/v020/20/heise.htm.
- Kipurry, N. (2000). *Oral literature of the Maasai*. Dar es Salaam: Ujuzi Educational Publishers.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: MoconPrinting Press.
- Njogu, K., na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo

Kenyatta Foundation.

Okpewho, I. (1992). *African Orala Literature Backgrounds, Characters and Continuity*, Bloomington and Indiana Polis: Indian University Press.

Odun, E. (1971). *Fundamental of Ecology Philadelphia*. Makala kutoka <http://www.researchgate.net>.

Ogechi I.U. (2015). Nature in Nigerian Childrens Literaturure:An Appraisal of Selected Verses. Tasnifu ya Umahiri, Ahmadu Bello, Zaria.

Payne, M., &Barbara, R. (2010).*Dictionary of Cultural and Critical Theory*. Wiley: Blackwell Publishers.

Thirmurthy, A.M. (2004). *Principle of Environmental Sciences, Engineering and Management*. Mumbai: Shroff Publishers.

Wamitila, K. W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited.

Akisiko la Hali na Mtazamo Hasi wa Maendeleo ya Mwanamke katika Jamii: Mifano Kutoka katika Riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad*

By

Hadija Rashid Utukulu & Omary Mohamed Maguo

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
hadijautukulu2@gmail.com

Ikisiri

Makala haya yamechunguza hali na mtazamo hasi wa maendeleo ya mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya Kiswahili. Data za msingi zimepatikana katika riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad* kwa mbinu ya usomaji makini. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kufafanua data za msingi zilipatikana kwa mbinu za kieletroniki na kimaktaba. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Ufeministi. Makala haya yanaelezea namna mwanamke anavyoakisiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii kupitia utanzu wariwaya ya Kiswahili. Aidha, inadokeza hali halisi ya maisha na matokeo ya harakati za mwanamke pamoja na namna jamii inavyomtazama katika maisha yake ya kila siku. Makala haya yanalenga kuchochea mwamko thabiti wa fikira zake ili kunyanyua na kutetea nafasi, hadhi na thamani ya kiutu anayostahiki katika ngazi na asasi mbalimbali za kijamii. Makala hii inahitimisha kuwa mwanamke hapaswi kutazamwa katika hali ya kupuuzwa na kukandamizwa badala ya kumtazama kama mhimili thabiti katika mifumo ya malezi, uzalishaji mali na uchumi katika ngazi zote za jamii na taifa.

Maneno Msingi: Hali, Hadhi, Mtazamo Hasi, Mwanamke na Fasihi ya Kiswahili,

1.0 Utangulizi

Fasihi ya Kiswahili iimejengwa katika uwanja mpana unaohakiki hali na harakati za maisha ya kila siku ya jamii hapa nchini na kwingineko barani Afrika. Kupitia utanzu huo, suala la maisha ya binadamu limejadiliwa kwamielekeo na maoni tofauti. Maisha ya binadamu yamechunguzwa katika ngazi zote za maisha yake tangu uzazi, malezi, ndoa, uzee hadi kifo (Fakih, 2017). Kila ngazi katika maisha ya binadamu ina harakati zake. Hali hiyo inatokana na kwamba kila jamii ina vikwazo vyake, miiko yake na masharti yake yanayomwongoza binadamu. Kanuni za jamii humfunga binadamu kuingilia matakwa na shughuli zake za kujiendeleza kimaisha na kimtazamo. Katika harakati hizo, binadamu wana matatizo yao, matakwa yao na maslahi yao yanayojidhihirisha katika kazi za fasihi.

Historia ya kudunishwa kwa mwanamke katika jamii za ulimwengu ni ndefu kwani inarudi nyuma hadi enzi zile jamii ya watu ilipoanza kugawanyika katika matabaka. Katika baadhi ya jamii kulikuwa na vipindi vya kihistoria ambamo wanawake walitawala kiuchumi na kisiasa

(Mapunjo, 2014). Hali hii ilitokea jamii ilipoanza kugawanyika na kutokea wale waliomiliki njia za uzalishaji mali na uchumi; ndipo mwanaume alipoanza kuwakilisha nguvu za uchumi na kuzitumia nguvu hizo kufanya lolote dhidi ya mwanamke. Uhusiano huo ulizidi kukuzwa na taasisi mbalimbali za kijamii, hasa za kidini na kindoa zilizoambatana na utoaji wa mahari. Suala la mahari linatazamwa katika misingi ya kumnunua mwanamke hali inayoendelea kumpa mwanaume wigo mpana wa kumtumia kwa namna anavyotaka.

Hali ya kupuuzwa kwa mwanamke katika jamii imefungamana na mkabala wa mwanamke kutumiwa kama chombo cha duni cha uzalishaji mali na kuendeleza kizazi katika jamii ya mwanadamu. Hali hii inatokana na sababu za kiutamaduni na fikra potofu zilizoshamira katika jamii kuhusu hali na hadhi ya mwanamke katika jamii (Githuci, 2013). Utatuzi wa mgogoro huo una mikabala mingi kufuatana na mitazamo ya jamii. Aidha, suala la usawa na ukombozi wa mwanamke halina misingi imara ya kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa; na uduni wake unajitokeza wazi wazi katika asasi mbalimbali za kijamii. Wanaume wanaendelea kuwasilisha nguvu za kiuchumi na kimadaraka katika asasi mbalimbali za kijamii na kitaifa.

Hali ya wanaume kuendelea kuwasilisha nguvu za kiutamaduni na kiuchumi imewafanya wanazuoni wengi kuichunguza nafasi ya mwanamke kupitia kazi za fasihi. Kwa mfano, Massoud (2018) anaeleza kuwa suala la ujinsia halijashughulikiwa vya kutosha katika uhakiki wa kifasihi, hasa katika fasihi za Kiafrika, ikiwamo fasihi ya Kiswahili. Wahakiki wengi wa fasihi za Kiafrika wanakumbana na wanawake katika miktadha mbalimbali, lakini wanakwepa kuchunguza na kuhakiki uhusika wao katika fasihi ya Kiswahili kutokana na kuwepo kwa sababu mbalimbali. Wasanii wengi wanamchora mwanamke katika sura mbalimbali kulingana namielekeo na maoni tofauti katika fasihi ya Kiswahili.

Baadhi ya wataalamu wamemtazama mwanamke kama mfungwa anayewekwa ndani muda wote pasipo kupewa ruhusa ya kutoka nje. Hali hiyo inamfanya mwanamke kunyimwa haki zake za msingi, pamoja na uhuru wa kutembea kutoka eneo moja kwenda eneo jingine. Jambo hilo lilimfanya Ruto (2015) kuzishambulia na kuzikosa baadhi ya asasi zinazochangia kuendelea kumdhalilisha na kumdunisha mwanamke katika jamii. Suala la kudhalilishwa na kudunishwa kwa mwanamke linapatilizwa na Sungi (2011) anapoeleza kuwa kuna mtazamo potofu ulioanzishwa na asasi za kijamii za kumwona mwanamke kama chanzo cha uovu katika jami bila kuchunguza kwa kina mchango wa mwanaume katika kumfanya mwanamke aoneshe tabia zisizofaa. Hali hii inasababishwa na kutamalaki kwa mifumo ya utamaduni inayomtaka mwanamke awe mnyenyekevu na mtiifu kwa mumewe.

Wapo waandishi wanaosisitiza kuwepo kwa usawa kati ya mwanaume na mwanamke katika jamii. Hali hiyo huwafanya wanawake wengi kupata nguvu na sauti katika maeneo mengi jambo linalosababisha kujengwa kwa jamii inayoanza kuweka misingi ya usawa na haki katika jamii

nyingi hapa nchini na kwingineko barani Afrika. Hali hiyo ilimfanya Lyatuu(2011) kueleza kwamba wanawake lazima wasimame kidete kwa nguvu zao ili wajitete na kupambana kwa dhati kwa sauti zao wenyewe na kuacha kuwategemea wanaume ambao kimsingi ndiyo wanaodhulumu haki wanazopigania. Wanawake hawana budi kupigania haki zao katika taifa lao ili kuhakikisha kuwa elimu, kazi, afya na huduma za kiuchumi zinatolewa kwa usawa. Kupigania haki zao ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi katika maeneo ya ngazi za maamuzi pasipo kubaguliwa.

Wahakiki na watafiti wengi wamejaribu kwa kiasi fulani kushughulikia suala la mwanamke kwa namna mbalimbali. Wengi wanaelekea kuafiki kuwa miundo ya kijamii pamoja na asasi zake inaashirikiana kumkandamiza mwanamke. Suala la utamaduni linatazamwa kama mhimiri mkuu unaosababisha kumdunisha mwanamke katika jamii (UN, 2014). Mifumo ya kiutamaduni iliyopo katika jamii imechangia kumchora mwanamke katika mitazamo chanya na hasi. Huu ndio msingi wa makala hii iliyolenga kuchunguza hali na mtazamo hasi wa maendeleo ya mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya Kiswahili.

2.0 Mbinu na Nadharia ya Utafiti

Makala haya yamechunguza hali na mtazamo hasi wa maendeleo ya mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya Kiswahili. Data za msingi zimepatikana katika riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad* kwa mbinu ya usomaji makini. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kufafanua data za msingi zilipatikana kwa mbinu za kieletroniki na kimaktaba. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Ufeministi. Mtazamo wa Ufeministi una historia ndefu duniani kwa kuwa uliibua vuguvugu la kutaka kufuta kabisa suala la uonevu dhidi ya mwanamke. Agenda ya Ufeministi inalenga kumaliza utawala wa mwanamke dhidi ya mwanamke. Ili kufanikiwa, wanawake wanahitaji kubomoa kabisa miundo ya mihimili ya utamaduni wa jamii iliojengeka katika sanaa, dini, sheria na kaya zinazodhibitiwa na mfumo wa kibaba na taswira zote za asasi zinazomwona mwanamke kama mtu dhaifu.

Katika makala hii, riwaya teule zilichunguza namna sura ya mwanamke inavyoaminika na kukubalika katika jamii ya wakati wake. Nafasi ya mwanamke ilichambuliwa na kuhakikiwa kulingana na uhusiano wa moja kwa moja uliopo kati ya jamii na hali halisi iliyopo katika jamii za Tanzania. Hali hii ni kwa sababu kazi ya fasihi inadhibitiwa na miundo iliyopo katika jamii kwa kuzingatia uhusiano wa wanajamii katika mienendo yao ya maisha yao ya kila siku. Riwaya teule itachunguzwa kama zao mahususi la jamii hiyo kwa kuzingatia historia yao, falsafa zao, mila na desturi zao, uchumi na siasa zao; na zilichunguzwa kama kiungo maalumu cha mahusiano ya kijamii. Nadharia hii imetumika kuchunguza hali, hadhi na maendeleo hasi ya mwanamke yanavyoakisiwa katika fasihi ya Kiswahili.

3.0 Mtazamo Hasi wa Mwanamke Unavyoakisiwa katika Riwaya Teule

Makala haya yamechunguza hali, hadhi na maendeleo hasi ya mwanamke yanavyoakisiwa katika fasihi ya Kiswahili. Uchunguzi umeonesha namna mwanamke anavyotazamwa katika jamii kwa kujikita katika riwaya teule. Katika riwaya teule suala la nafasi hasi ya mwanamke inavyoakisiwa limechunguzwa katika sura mbalimbali kama ilivyoelezwa katika sehemu inayofuata.

3.1 Haki ya Kushiriki katika Shughuli za Uzalishaji Malina Uchumi

Katika baadhi ya jamii, inaaminika kuwa shughuli za uzalishaji mali na uchumi ni jukuu la mwanaume pekee na si mwanamke. Jambo hilo linasababisha kuzorota kwa maendeleo ya mwanamke, familia na taifa kwa ujumla kwa kuwa mwanamke ni mzalishaji mkuu katika jamii nyingi barani Afrika. Hali inamfanya mwanamke awe tegemezi katika masuala mbalimbali ya usimamizi wa familia na maisha yake mwenyewe. Kuendelea kufanya hivyo ni kuendelea kumnyima fursa pana ya kushirika katika maendeleo ya jamii na taifa lake. Mbiu (2013) anasisitiza kuwa jamii inapaswa kutambua kuwa suala la uzalishaji mali na uchumi halipaswi kuegemezwa upande mmoja tu mwanaume na kumwacha mwanamke nyuma kabisa ili kuyafikia maendeleo na kujenga jamii endelevu. Mwandishi anaeleza:

Inasemwa mara kwa mara kwamba katika maisha mwanamke alikuwa na mapigano mengi kama mwanaume. Kama hili lilikuwa si mzaha wa kupitisha wakati, basi ilikuwa wajibu wa kila nchi kuandaa wanawake wote kwa mapigano yao. Kufaulu kwao kulikuwa kushindwa kwa watu wote. Umati wa wanawake wa kazi na matendo mbalimbali kama Siti alivyokuwa ndilo jeshi lililotakiwa katika wokovu wa maisha katika Afrika Mashariki (Uk. 58),

Ufafanuzi huo unasisitiza kuwa suala la uzalishaji mali na uchumi katika jamii ni umhimu kufanywa na kuwa katika mikono ya mwanamke na mwanaume ili kuleta maendeleo ya haraka ya kiuchumi katika jamii. Ushirikiano wa pande mbili utajenga umoja thabiti wa kufanya kazi kwa manufaa ya kuendeleza familia na taifa lao. Umoja ni fimbo ya mnyonge. Suala la umoja na bidii katika uwajibikaji ni miongoni mwa mambo ya msingi katika kuinua uchumi wa familia, jamii na taifa. Uwajibikaji ni nyenzo muhimu katika kuyamudu mahitaji ya msingi (Mabuba, 2015). Pia, huiasa jamii kufanya kazi kwa umoja, mshikamano na bidii. Umoja ni fimbo ya mnyonge katika jamii na taifa lolote. Umoja na shina la maendeleo, na ni silaha bora dhidi ya umaskini.

Katika mfumo wa biashara nchini, wanawake hawapati mikopo kwa urahisi kama jitihada mojawapo ya kumudu harakati zao za kibiashara. Wengi wao hawana uwezo wa kuendesha biashara zao katika kiwango kinachofaa kutokana na kukosekana kwa mitaji inayokidhi harakati zao za msingi (Sanga, 2013). Pia, wanawake hawakopesheki na hawaaminiki katika taasisi zinazojihusisha na masuala ya fedha kutokana na kuwapo kwa sababu mbalimbali. Wengi

hawafanyi biashara zao kisasa kutokana na ukosefu wa mitaji yenye tija. Pengo linalobainishwa huwafanya wanawake walio wengi kutokuwa na sauti katika maeneo mengi.

Aidha, ipo haja ya kujenga vyombo na taratibu zitakazojali nafasi za maumbile katika shughuli za maendeleo. Miundo ya mikakati, mitazamo ya ushirikishaji wa kiwakati na kisera, mafunzo ya mawakala wa maendeleo na marekebisho ya taratibu za uendeshaji na za sheria, lazima vyote vioneshe jukumu muhimu walilionalo wanawake katika kujenga uchumi wa jamii na taifa, hasa katika shughuli za uzalishaji mali na uchumi katika ngazi zote za kijamii. Fikira hizo zinahitajika kubadilika katika jamii zote, hasa katika jamii ambazo hisia za mwanamke kuwa duni kuliko mwanaume zinaendelea kutamalaki, na ambako hirizi ya utamaduni mbovu unaoendelea kutumiwa kuhalalisha kubaguliwa kwao (Maganga, 2016). Kwa kutambua majukumu ya maendeleo ya taifa, lazima wanawake washirikishwe na kuwezesha kikamilifu katika shughuli zote za maendeleo ya jamii na taifa.

3.2 Haki ya Kujishughulisha na Sanaa Muziki

Kutokana na kuwepo kwa imani potofu zilizoshamiri katika baadhi ya jamii hapa nchini na kwingineko barani Afrika, mwanamke hakuruhusiwa kujishughulisha na masuala yanayohusiana na sanaa. Mwanamke alidiriki kufanya hivyo alitazamwa kama malaya. Jambo hilo lilisababisha kuwanyima wanawake kushiriki kikamilifu katika masuala ya kiutamaduni na hata kudumaza vipaji vyao na kukosa kipato cha kujikimu kwa sababu sanaa ni sehemu ya ajira. Hali ya kumchukulia mwanamke kama malaya akishiriki katika masuala ya sanaa na utamaduni katika jamii yake, lilimfanya Kitundu (2012) atoe kauli ya kuacha tabia kumpuuzwa mwanamke na kumdhalilisha kiutamaduni. Pia, alionesha kuwa bado mwanamke anapewa nafasi duni inayomdhalilisha mwanamke kama chombo cha starehe, malaya, mchawi ama kiumbe dhaifu. Katika riwaya teule mwandishi anaonesha namna Siti alivyokuwa na kipaji cha sauti, lakini hakujua jinsi ya kukitumia vema kutokana na kuwepo kwa imani potofu katika jamii yao. Mwandishi anaeleza:

Siti alikuwa na kipawa cha sauti, lakini alikuwa hajui jinsi ya kukikuza wala kukipalilia. Pia, hakujua jinsi ya kushika pahali pake katika tamasha. Alikuwa hana msingi wowote wa kujengea kuta za ustawi wake (Uk. 11).

Maelezo haya yanaonesha kuwa wanawake wengi katika jamii za Kiafrika wana vipaji vya uimbaji katika tasnia ya muziki na sanaa, lakini hawapewi nafasi kutokana na kuwepo na kushamiri kwa imani potofu zinazomtazama mwanamke mwanamuziki ni mhuni, malaya na hawezi kumudu harakati za malezi ya familia yake. Jamii inapaswa kuelewa kuwa mwanamke anahitaji kupata fursa pana ya kujiendeleza kiuchumi na kijamii kwa kujiari kupitia fani ya muziki na sanaa. Hoja hii inapewa uzito na Omary (2009) anayesisitiza kuwa sanaa ya muziki ni sehemu ya ajira kwa wasanii na wadau wengine wanaojihusisha na kazi za kisanaa. Mtazamo

